

MAJIBU YENYE FAIDA NO.4

KUHUSU

MASWALI YANAYO FUNGAMANA NA MIFUMO MIPYA

MTUNZI, SHEIKH SWALEH BIN FAWZAN BIN ABDILLAH AL FAWZAN

MFASIRI, ABUL 'AALIYAH 'UMAR BIN MUHAMMAD BIN KONDO

PONGWE - TANGA - TANZANI

Swali la nne: Tunasikia mengi kuhusu yale ambayo huitwa “makundi ya kiislamu” katika zama hizi katika sehemu mbalimbali ulimwenguni, je..! ni ipi asili ya huku kuitwa? Na je..! itafaa kuondoka nao na kushirikiana nao ikiwa hawana bid’ah (uzushi katika Dini)?

Jibu: Mtume swala na salamu zimshukie jametueleza na ametubainishia namna gani tutende, hakuna kitu chochote alichokiacha kitakachoukaribisha umma wake kwa Allah isipokuwa ameshakibainisha, na hakuna kitu alichokiacha kitakacho uweka mbali umma wake na Allah isipokuwa ameshakibainisha swala na salamu zimshukie.

Na mionganini mwa hayo ni mas'ala haya. Amesema Mtume swala na salamu zimshukie : (*Hakika hali na shani ilivyo atakae ishi mionganini mwenu ataona tofauti nydingi...)* –lakini ipi tiba itakapotokea tofauti hiyo? – amesema : (*Basi lazimianeni na sunna zangu na sunna za makhalifa waongofu waliyo ongoka baada yangu, shikamaneni nazo na ziumeni kwa (meno ya) magego ,na tahadharini na mambo yaliyozushwa kwa sababu kila kilichozushwa ni uzushi,na kila uzushi ni upotevu¹*)

Basi haya makundi, kuna katika hayo yapo juu ya uongofu wa Mtume swala na salamu zimshukie na uongofu wa maswahaba wake, na hasa makhalifa waongofu na karne bora, basi kundi lolote lililokuwa juu ya njia hii sisi tupo pamoja na kundi hilo,

¹ -Ameipokea Imamu Abuu Dawd (4607) na Imamu Tirmidhiy (2676) na ameisahihisha sheikh Al Albaniy katika kitabu chake “al Ir’waau al ghaliil (2455)

tutajinasibisha nalo, na tutafanya nalo ‘amali pamoja nalo.

Na lile lililo kwenda kinyume na uongofu wa Mtume swala na salamu zimshukie-hakika tutajiepusha nalo hata kama lijiite “kundi la kiislmau” mazingatio hayakuwa katika majina (kujiita na kujinasibu tu), bali mazingatio ni kwa hakika, ama majina huwenda yakawa makubwa lakini hayana kitu, hakuna humo chochote au vilevile yanaweza kuwa batili.

Na amesema Mtume swala na salamu zimshukie: (*Wametofautiana Mayahudi juu ya makundi sabini na moja, na wametofautiana Manaswara juu ya makundi sabini na mbili, na utatofautiana Umma huu juu ya makundi sabini na tatu, yote ni motoni isipokuwa kundi moja, tukasema (sisi maswahaba). ni kina nani hao ewe Mtume wa Allah? akasema: ni*

*wale watakaokuwa juu ya mfano wa yale ambayo
mimi nipo juu yake leo hii na Maswahaba zangu* ²).

Njia iko wazi,basi kundi ambalo lina alama hii tutakuwa nalo,nao ni wale waliokuwa juu ya mithili yale aliyokuwa nayo Mtume na Maswahaba zake, basi wao ndio kundi la kiislamu la kweli.

Ama atakae halifu hii manhaji (njia au mfumo),na akapita njia nyingine hakika huyo si katika sisi na sisi si katika yeye na wala hatujinasibishi na yeye,na yeye hajinasibishi na sisi na hataitwa jama'ah bali ataitwa yeye ni katika pote mionganoni mwa mapote yaliyo potea,kwa sababu jama'ah haiwi ila juu ya haki,nayo ni haki ambayo wanakusanyika juu ya haki hiyo watu,na ama batili hakika yake inafarikisha wala haikusanyi, amesema Allah hali ya

² - Ameipokea Imamu Tirmidhiy (2641) na Imamu ibn Maja (3992) na Imamu Abuu Dawd (4597)

kuwa ametukuka: (*Na wakikengeuka basi wao wamo katika upinzani tu*³.)

³ - Suratu-al- Baqarah aya 137